

Public Disclosure Authorized  
Public Disclosure Authorized  
Public Disclosure Authorized  
Public Disclosure Authorized  
Public Disclosure Authorized



# KUELEWEKA WAZI:

Sera faafu za Lugha ya Ufundishaji  
Kwa ajili ya Kujifunza

## **SHUKURANI**

*Makala hii iliandikwa na kikundi kilichoongozwa na Michael Crawford na Sergio Venegas Marin, chini ya uelekezi wa Jaime Saavedra na Omar Arias, na ikijumuisha Penelope Bender, Barbara Trudell, Djir Jhingran, Huma Kiswai, Elaine Ding, Laura Gregory, Lisha Almeida, AMberine Huda, Ashwarya Khurana, na Tihtina Zenebe Genre. Makala hii ilihaririwa na John Steinhardt. Kikundi hiki kilinufaika kutoka kwa maoni ya Reema Nayar, Jason Allen Weaver, Adelle Pushparatnam, Samer Al-Samarrai, Lianqin Wang, Tara Beteille, Toby Linden, Harry Patrinos, Hanna Katriina Alasuutari, Juan Manuel Moreno, Marguerite Clarke, Melissa Adelman na washiriki wengine wa Mpango wa Educational Global Practice ambao walishiriki katika majadiliano kuhusu makala hii. Michoro na usanifu ulielekezwa na Nicole Hamam na michoro iliandaliwa na Margaret Flatley.*

# Muhtasari Mkuu wa Makala

---

**ULIMBIKIZAJI WA MTAJIWATU PAKUBWA NI JITIHADA INAYOJIKITA KWENYE LUGHA.** Ndio msingi wa mali katika jamii za kisasa na kimsingi hupatikana kupitia kwa mafunzo shuleni. Sera zinazolenga kuhakikisha wingi wa idadi na ubora wa mtajiwatu zina athari chanya kwa wingi. Ili kuhakikisha manufaa yake, mataifa sharti yazidishe kujifunza katika shule, na kwa kufanya hivyo yainue Kipimo cha kutathmini kiwango cha ubora wa kujifunza na kiasi cha kujifunza (LAYS) cha watu wake. Benki ya Dunia imeunda Mradi wa Mtajiwatu na Kipimo cha Mtajiwatu ili kuangazia haja ya kisera ya nchi mbalimbali kuwekeza katika watu wake na haja ya watu kuwekeza katika maisha yao binafsi. Sera zinazokuza ulimbikizaji wa mtajiwatu - kama vile sera nzuri za lugha ya ufundishaji-zinapaswa kukuzwa na Benki ya Dunia na ziwe muhimu katika mijadala ya nchi inayohusu kuwasaidia watu kufikia uwezo wao kamili.

**CHA KUSTAAJABISHA NI KUWA MATOKEO YA VIWANGO VYA CHINI VYA KUJIFUNZA HUENDA YANAAKISI SERA ZA LUGHA YA UFUNDISHAJI ZENYE UPUNGUFU.** Kipengele cha LAYS katika Kipimo cha Mtajiwatu na vipimo vya umasikini wa kujifunza vinadhihirisha viwango vya chini sana vya ujifunzaji. Katika baadhi ya nchi, watoto waliohudhuria masomo ya msingi kwa miaka mitatu hawawezi kutambua hata neno moja lililoandikwa, na huenda wakatambua herufi moja tu. Bila kuzingatia masuala ya lugha ya ufundishaji, mtu anaweza kuhitimisha kimakosa kwamba walimu hawana ufahamu na stadi za kufundisha, au kwamba wanafunzi hawana uwezo wa kujifunza kabisa. Fikira mbadala zenye mantiki ni kwamba walimu wanahitajika kufundisha katika lugha ambayo wanafunzi hawasemi au kuelewa. Matokeo ya chini ya mitihani katika baadhi ya hali yanaakisi kiwango cha kutoelewa lugha inayotumiwa kufundisha na/au kutahini; hayaakisi upungufu wa kujifunza katika hali zinazofaa.



**SERA FAAFU KUHUSU LUGHA YA UFUNDISHAJI HURAHISISHA KUJIFUNZA NA MASUALA MENGINE.** Watoto wanapofundishwa kwa kutumia lugha ambayo wanaisema na kuelewa vyema wanajifunza zaidi, wana nafasi nzuri ya kujifunza lugha zingine, wana uwezekano mkubwa wa kusalia shuleni, na kufurahia tajriba wanazopitia shuleni kuambatana na utamaduni na hali zinazohusika. Kongoo pana na ya kutosha ya utafiti, iliyorejelewa kote katika makala hii, inathibitisha ukweli huu. Sera faafu za lugha ya ufundishaji pia huchangia usawa shuleni na katika soko la ajira, hupunguza gharama za elimu, na kusaidia kuhakikisha nafasi sawa. Sera nzuri zinazohusu lugha ya ufundishaji ni nguzo ya mikakati ya kitaifa ya uendelezaji wa mtajiwatu, na kwa jinsi hiyo inapaswa kuwa shauku muhimu kwa waunda sera wa kitaifa na wadau katika maendeleo.

**SERA NZURI ZA LUGHA YA UFUNDISHAJI HAZIJATILIWA MKAZO IPASAVYO.** Licha ya manufaa yake mengi, mifumo mingi ya elimu haitekelezi sera faafu kuhusu lugha ya ufundishaji. Badala yake, mara nyingi watoto hujifunza kupitia lugha ambazo hawazifahamu vyema - na, katika hali nyingi, katika lugha ambazo hawazifahamu kamwe. Watoto wanaoathiriwa na sera hizi aghalabu wana changamoto nyingine kama vile hadhi ya kijamii na kiuchumi na umbali kutoka kwenye miji. Hali ambayo hufanya ujifunzaji na maendeleo shuleni kuwa changamoto. Kuwahitaji walimu kufundisha katika lugha ambayo wao na wanafunzi wao hawasemi ni desturi ya kawaida licha ya ushahidi kuwa asilimia 90 au zaidi ya wanafunzi huenda wakakosa kupata stadi za kimsingi kama vile uwezo wa kimsingi wa kusoma, kuandika na kuhesabu wakiwa katika shule ambazo zinatekeleza sera hizi.

**SERA ZISIZOFAA ZA LUGHA YA UFUNDISHAJI HUDHURU UJIFUNZAJI, UFIKIAJI, USAWA, GHARAMA, NA UJUMUISHAJI.** Kiasi kikubwa na kinachozidi kuongezeka cha tafiti kinaonyesha kuwa watoto hujifunza vyema zaidi katika lugha yao ya kwanza (L1) kushinda katika lugha yao ya pili (L2). Wanapofundishwa katika L1 kwanza, wanaongeza uwezekano wao wa kuwa na ustadi katika L2 na kupokea mafunzo ya kiakademia pasi na tatizo. Isitoshe, wanaongeza uwezekano wao wa kusalia shuleni, Watoto kutoka kwa familia zilizomo kwenye asilimia 40 ya chini katika msambao wa kijamii na kiuchumi wana uwezekano mkubwa wa kuvumilia mafunzo katika lugha ambayo hawaelewi, na wanakosa rasili-mali katika familia za kuwasaidia kukabiliana na athari za sera zisizofaa kuhusu lugha ya ufundishaji katika shule wanazohudhuria. Nchi zinazotumia sera za lugha ya ufundishaji zinazohimiza matumizi ya lugha ambazo hazisemwi wala kueleweka na walimu na wanafunzi hupata matokeo duni kutoka kwa uwekezaji katika elimu. Sera hizi huchangia ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaoacha kuhudhuria shule, kiwango cha kurudia madarasa, na kiwango cha chini cha kujifunza kwa ujumla. Kwa mantiki hii, nchi zingenufaika kifedha iwapo, kwa kufuata sera bora zaidi za lugha ya ufundishaji, zingepunguza gharama ya kuelimisha kila mwanafunzi anayekamilisha masomo yake na kila kipengele cha ujifunzaji kilichoeleweka. Hali hii pia ingefanya elimu kuwa faafu kwa wanafunzi na kuwahusisha wanafunzi kwa njia mbalimbali, ikiwemo thamani iliyomo na hadhi ambayo lugha hupata inapotumiwa kama mbinu rasmi ya kufundishia.

**SERA ZISIZOFAA ZA LUGHA YA UFUNDISHAJI ZINAATHIRI TAKRIBAN ASILIMIA 37 YA WANAFUNZI KATIKA NCHI ZENYE UCHUMI WA CHINI NA UCHUMI WA KATI.** UNESCO (2016) inakadiria kwamba ulimwenguni wanafunzi wanne kati ya kila wanafunzi kumi wanafundishwa katika lugha ambazo hawazijui. Ithibati kutoka kwenye uchanganuzi asili uliofanywa katika makala hii pakubwa ulithibitisha idadi hii na unashuhudia ukubwa wa tatizo hili: Asilimia 37 ya wanafunzi katika nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati hawafundishwi katika lugha wanazosema na kuelewa vyema. Katika baadhi ya nchi, zaidi ya asilimia 90 ya wanafunzi wanafundishwa kwa lugha ambayo hawasemi wala kuelewa. Zaidi ya robo ya wanafunzi bilioni moja wanaathiriwa. Kwa mujibu wa data kutoka kwa Ethnologue, nchi 12

**Asilimia 37 ya wanafunzi katika nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati hawafundishwi katika lugha wanazosema na kuelewa vyema.**








katika ya 20 zilizo na kiwango kikubwa zaidi cha umasikini wa kujifunza hutumia lugha za Kufundisha ambazo wanafunzi wachache wanaelewa wanapoingia shuleni. Asilimia 53 ya watoto katika nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati wanaoshindwa kusoma na kuelewa kufikia umri wa miaka kumi karibu katika hali zote hujumuisha kiasi kikubwa cha wanafunzi amabo hawafundishwi katika L1.

**MAENDELEO MAKUBWA YANAWEZEKANA KWA KUFUNDISHA KATIKA IDADI NDOGO YA LUGHA ZA ZIADA.** Uwezekano wa kufundisha katika kila moja ya lugha zaidi ya 7,000 za ulimwengu unakatisha tamaa, lakini hisia hii imepotoka. Mijadala kuhusu sera aghalabu hutingwa na wazo kuwa kushabikia elimu inayotolewa katika lugha ya mama katika mazingira ya wingilugha (MTB-MLE) ni ghali na kutatabisha. Kwa hakika, elimu ya wingilugha inayojikita kwa lugha ya mama si ghali na ni rahisi kupanga kuliko inavyodhaniwa kwa kawaida. Kweli, wanafunzi wengi zaidi ambao kwa sasa wanapata mafunzo katika L2 wangufaika kutokana na upanuzi wa kilimwengu wa idadi ya lugha zinazotumiwa kufundishia. Robo tatu (asiliamia 75) ya tatizo hili huenda ikasuluhishwa kwa kutoa mafunzo katika lugha 220 zaidi kote ulimwenguni - kwa wastani ikiwa ni lugha moja ya ziada kwa kila nchi. Ili kufikia asilimia 84 ya wanafunzi wote wa lugha za wachache katika nchi zote kutahitaji kufundisha katika takriban lugha 559 pekee - chini ya lugha tatu za ziada kwa kila nchi. Katika hali hizi mbili, lugha mbazo zingengezwa tayari ni “lugha zilizo katika maandishi.” Zina othografia zilizostawi, na kila moja inazungumzwa na angalau wasemaji milioni 1.5. Lugha za ulimwengu takriban 6,200 zinazosalia zinazungumzwa na chini ya asilimia 10 ya watu wote ulimwenguni. Sehemu ya tano juu ya sita ya tatizo inaweza kusuluhishwa kupitia kwa juhudi za kimakusudi; kusuluhisha sehemu ya moja juu ya sita iliyosalia itahitaji uzidishaji maradufu wa muda na rasilimali.

**SERA ZA LUGHA YA UFUNDISHAJI ZINAATHIRIWA NA MASUALA YA KISIASA NA KIUCHUMI.** Kutokana na ushahidi huu, kwa nini nchi nyingi bado zinachagua lugha ya ufundishaji ambao inasababisha matokeo duni ya ujifunzaji na kusababisha utengaji wa kijamii? Mojawapo ya sababu huenda ikawa ni ukosefu wa ufahamu wa manufaa ya kufundisha katika lugha ambayo wanafunzi wanaisema na kuelewa vyema. Masuala mengine tunahoji hayana uelekevu sana. Chaguzi za lugha katika elimu aghalabu hutokana na uzingatiaji wa masuala ya kisiasa zaidi ya sekta ya elimu. Lugha inafungamana kwa karibu na utambulisho wa kitaifa na utambulisho wa kisiasa. Ujenzi wa taifa wakati mwingine hujumuisha ukuzaji wa lugha ya kikundi kimoja na kuacha lugha za vikundi vingine. Ustadi wa lugha una thamani katika soko la ajira. Wazazi aghalabu wana mtazamo kuwa umilisi katika lugha ya mjini au ya kimataifa ni muhimu kwa mafanikio ya watoto wao kitaaluma. Matokeo – malengo – kama vile ustadi katika L2 ya kimataifa, yanaweza kuongoza mbinu katika njia ambayo inaenda kinyume na matarajio wakati ambapo mafundisho yote yanatolewa katika lugha hiyo ya pili licha ya viwango vya ustadi wa mwalimu au mwanafunzi. Ni muhimu kuzingatia muktadha mpana kisiasa katika kudhukuru masuala ya sera faafu ya lugha ya ufundishaji.

**SULUHU ZA KISERA ZIPO ILA HAZITEKELEZWI KWA UTARATIBU.** Utetezi wa kuwepo kwa sera nzuri za lugha ya ufundishaji umekuwa ukiendelea kwa miongo mingi lakini umeteka makini ya wanaofanya maamuzi na wadau katika maendeleo mara chache mno. Mtindo wa kuwepo kwa tafiti nyingi na bora hata hivyo unaibuka katika baadhi ya maeneo. Tajriba zimeandaliwa muhtasari na unachanganuzi umeibua ushauri thabiti wa kisera kwenye suala hili kwa jumla na kwa takriban masuala yote madogo yanayohusika. Ushauri mzuri unapatikana kwa ajili ya uchanganuzi katika kiwango cha nchi na kusaidia upangaji wa lugha ya kutumiwa katika elimu. Miongozo na mifano ya upeo mzuri na mpangilio wa ufundishaji katika L1 ipo kwa wingi. Mbinu za kuandaa nyenzo za kufundishia na kujifunzia, ikiwemo programu za tarakilishi zinazoandaa vitabu vya kiada na vitabu vya hadithi za watoto zinapatikana bila malipo na zinatumiwa kwa wingi kushinda ilivyokuwa hapo awali. Chaguzi za kisera kuhusu masuala mbalimbali yanayoathiri walimu, ufundishaji, na ukufunzi zinazidi kukua. Ufahamu kuhusu masuala na shauku za lugha ya kutathmini unazidi kuongezeka. Ushahidi wa kisayansi kuhusu ufaafu wa “Kuacha polepole” (tazama hapo chini) na mikakati mingine faafu ya mitaala na ufundishaji inapatikana. Ingawa hivyo, maendeleo bado yanajikokota na nyenzo zilizopo hazifahamiki na kueleweka vyema.

**Kuboresha matokeo ya lugha ya ufundishaji kwa kanuni tano za kimsingi. Ushahidi uliotolewa katika makala hii unalenga kanuni tano muhimu ambazo kwa pamoja zinaunda mwelekeo mpya wa kuimarisha ujifunzaji katika nchi zenye uchumi wa chini na uchumi wa kati:**

KANUNI 1	KANUNI 2	KANUNI 3	KANUNI 4	KANUNI 5
 <p><b>Watoto wafundishwe katika L1 yao kuanzia kwa huduma za Elimu na Utunzaji wa Watoto Wadogo (ECEC) hadi angalau miaka sita ya kwanza katika shule ya msingi.</b></p> <p>Ni muhimu kwamba ufundishaji ufanywe katika lugha ambayo wanafunzi wengi wanasema na kuelewa vyema kabisa.</p>	 <p><b>Tumia L1 kwa ufundishaji wa masomo ya kiakademia zaidi ya kusoma na kuandika Wanafunzi wanapaswa kujua kuandika na kusoma katika taaluma mbalimbali na katika masomo yote yanayotolewa shuleni.</b></p>	 <p><b>Tanguliza L2 kama lugha ya kigeni ikilenga stadi za kusema lugha.</b></p> <p>Endelea kwa ujuzi wa kusoma na kuandika katika L2 na ufundishaji wa yaliyomo baada tu ya wanafunzi kupata ustadi wa kutosha katika ujuzi wa kusoma na kuandika katika L1 na uwezo wa kusema L2. Wanafunzi wanaweza kujua lugha mbili katika elimu ya msingi iwapo ufundishaji na mpangilio utafanywa kuwa bora.</p>	 <p><b>Endelea kufundisha L1 baada ya L2 kuwa lugha kuu ya kufundishia.</b></p> <p>Ufundishaji wa L1 unaendelea kuimarisha utendaji katika L2 kwa njia muhimu hata baada ya L2 kuwa lugha kuu ya ufundishaji.</p>	 <p><b>Endelea kupanga, kukuza, kurekebisha, na kuimarisha utekelezaji wa sera za Lugha ya ufundishaji, kuambatana na muktadha na malengo ya nchi.</b></p>

Makala hii inaeleza mwelekeo mpya wa kisera wa Benki ya Dunia kuhusu lugha ya ufundishaji, kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Sera ya Ujuzi wa kusoma na kuandika inayounga mkono Malengo mapya ya Ujifunzaji ya Benki hii. Mwelekeo huu mpya unalenga kusaidia ukuzaji wa sera za Lugha ya ufundishaji na uingiliaji, huku changamoto zinazotokana na lugha ya ufundishaji zikibainishwa na kushughulikiwa kwa kuzingatia muktadha wa kila nchi. Chini ya mwelekeo huu mpya, Benki ya Dunia inahimiza umuhimu wa kuchunguza kanuni zifuatazo ili kuimarisha ujifunzaji katika mataifa yenye uchumi wa chini na uchumi wa kati:

- **Kanuni 1** Watoto wafundishwe katika L1 yao kuanzia kwa huduma za Elimu na Utunzaji wa Watoto Wadogo (ECEC) hadi angalau miaka sita ya kwanza katika shule ya msingi. Ni muhimu kwamba ufundishaji ufanywe katika lugha ambayo wanafunzi wengi wanasema na kuelewa vyema kabisa.
- **Kanuni 2** Tumia L1 kwa ufundishaji wa masomo ya kiakademia zaidi ya kusoma na kuandika Wanafunzi wanapaswa kujua kuandika na kusoma katika taaluma mbalimbali na katika masomo yote yanayotolewa shuleni.
- **Kanuni 3** Tanguliza L2 kama lugha ya kigeni ikilenga stadi za kusema lugha. Endelea kwa ujuzi wa kusoma na kuandika katika L2 na ufundishaji wa yaliyomo baada tu ya wanafunzi kupata ustadi wa kutosha katika ujuzi wa kusoma na kuandika katika L1 na uwezo wa kusema L2. Wanafunzi wanaweza kujua lugha mbili katika elimu ya msingi iwapo ufundishaji na mpangilio utafanywa kuwa bora.
- **Kanuni 4** Endelea kufundisha L1 baada ya L2 kuwa lugha kuu ya kufundishia. Ufundishaji wa L1 unaendelea kuimarisha utendaji katika L2 kwa njia muhimu hata baada ya L2 kuwa lugha kuu ya ufundishaji.
- **Kanuni 5** Endelea kupanga, kukuza, kurekebisha, na kuimarisha utekelezaji wa sera za Lugha ya

ufundishaji, kuambatana na muktadha na malengo ya nchi. Benki ya Dunia inapaswa kushirikiana kwa karibu na nchi husika na wadau katika maendeleo kuunda na kusambaza rasilimali pamoja na kuhimiza nafasi zenye ubora wa hali ya juu za kujifunza ambazo ni faafu kwa mujibu wa sera za lugha ya ufundishaji.

Ili kukuza na kutekeleza mwelekeo huu, Benki ya Dunia inapendekeza mihimili mitatu ya kazi ambayo itahakikisha kuwa kanuni hizi zinajumuishwa kwa utaratibu katika shughuli za Benki ya Dunia. Mhimili 1 unajikita kwa uchanganuzi na tathmini ya hali za lugha ya ufundishaji katika kila nchi inayohusika pamoja na chaguo kuu za sera zilizopo. Mhimili 2 unahusisha ushiriki wa kimakusudi katika masuala ya lugha ya ufundishaji kupitia kwa mijadala iliyokuzwa na kupanga kusaidia nchi kushughulikia masuala yaliyopewa kipaumbele. Kama sehemu ya Mhimili 3, mpango wa Benki wa Education Global Practice utashirikiana na wadau wengine kuhimiza makini inayofaa kwa masuala ya lugha ya ufundishaji na katika kuunda, kuku-sanya na kusambaza ufahamu wote wa kisasa na suluhu za kisera na kukuza suluhu za kudumu kwenye masuala ya lugha katika elimu.

**AZMA, HADHIRA, UPEO NA MUUNDO WA MAKALA HII.** Azma yake ni kuhakikisha kwamba Mpango wa Benki ya Dunia wa Education Global Practice unaweza kuwasaidia wateja kukabili au kuondoa mata-tizo sugu ambayo yanatokana na sera zisizofaa za lugha ya ufundishaji kwa ajili ya ujifunzaji na mfumo wa elimu. Makala hii ni fupi kimakusudi, si makala kamili ya kiakademia. Taarifa za kutosha zimetolea ili kuanza kueleza masuala kwa kuzingatia maamuzi ya sasa ya kisera, sio kuangazia suala hili kwa ujumla. Makala hii imechagua vipengele na haijaangazia lugha ya ufundishaji kwa kujikita kwa vipengele vyote vya sera ya elimu. Haijaangazia dhima ya lugha ya ufundishaji katika elimu ya juu, vyo anuwai, elimu kwa watu wazima, au ujifunzaji wa maisha yote. Makala inapendekeza kuidhinishwa kwa mwelekeo mpya kutoka kwa usimamizi wa Benki ya Dunia. Kukubali mapendekezo yake kutajumuisha kujitolea kuchukua hatua mbalimbali ambazo zitasaidia nchi wanachama wa Benki ya Dunia, ikiwemo uchanganuzi wa kina zaidi, ukuzaji na usambazaji wa bidhaa za umma kwa ulimwengu, kuimarisha ufahamu na ujuzi wa wahudumu katika sekta ya elimu na mijadala madhubuti zaidi, hasa katika elimu ya msingi. Wasomaji wanapaswa kuzingatia kuwa:

- ***Bado hatuna majibu yote.*** Kadri tunavyosonga mbele, mapengo katika ufahamu tulionao yatahitaji kushughulikiwa na kujazwa. Kwa mfano, tutahitaji kuelewa vyema zaidi na kuibuka na mapende-kezo ya kuimarisha hali bora za pili, kama zile zinazohusisha mzamo wa L2 moja kwa moja. Vivyo hivyo, masuala mengine yanayochangia upungufu wa ustadi miongoni mwa walimu katika lugha lengwa pamoja na ustadi wa chini wa wanafunzi yanapaswa kudavuliwa. Athari za muda unao-tumika kwa zoezi, ubora wa nyenzo za ufundishaji na kujifunzia, msaada kwa walimu na masuala mengine yanaunda ajenda ya siku zijazo ambayo inahitaji kuangaziwa kwa haraka iwapo ushauri wa kisera utaboreshwa.
- ***Uongozi huhitaji Kujitolea kwa uendelevu*** Masuala ya lugha ya ufundishaji yanaweza kudhibiti-wa lakini hayawezi kusuluhishwa kikamilifu. Juhudi za kisera za nchi zinapaswa kuwa sehemu ya kawaida ya sera ya jumla ya elimu. Kujitolea kwa uendelevu kwa upande wa wadau katika maende-leo, huku Benki ikilenga kutoa mfano kama mdau muhimu, pia kunapaswa kuwa sehemu ya juhudi za jumla za kuimarisha ujifunzaji.

Sehemu 1 inaangazia kwa nini tunapaswa kujali masuala ya lugha ya ufundishaji na changamoto kuu zinazohusika. Vifungu vyake vinne vimepewa mada ifuatavyo: (i) Kwa nini tujali? (ii) Tatizo hili ni kubwa kiasi gani? (iii) Dhima ya uchumi wa kisiasa; na (iv) Miktadha anuwai ya Lugha ya ufundishaji. Sehemu 2 inawasilisha suluhu zilizopo (katika kifungu cha 5) na kupendekeza mustakabali kwa Mpango wa Benki ya Dunia wa Education Global Practice (kifungu cha 6) Ni muhimu kutambua kuwa makala hii haijadai kumiliki au kupendekeza mkusanyiko kamili wa suluhu za kiufundi kwa changamoto nyingi za masuala ya kisera zinazohusika. Kwa kuimarisha ushirikiano na kuwekeza rasilimali za kutosha kwa changamoto zilizopo, suluhu zilizopo zitatumiwa, na suluhu mpya kuibuliwa. Ongezeko la ushirikiano na kubadilis-hana mawazo kutakuwa sehemu muhimu, sawa na kufanya majaribio ya mielekeo mipya. Mwelekeo mpya utahusisha ujifunzaji katika kiwango cha kibinafsi na kiwango cha asasi, huku kiwango cha ushirikiano kikilingana na dharura ya suala linaloshughulikiwa.

